ewura

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji

ISO 9001: 2015 Certified

HALIUZWI

# Newsletter

FEBRUARI 2023

ISSN 1821 - 7273 TOLEO NA. 35

# EWURA YASHINDA TUZO YA UMAHIRI WA UHUSIANO BORA



**Kauli Mbiu:** *"Udhibiti wa Haki kwa Matokeo CHANYA - IMPACT"*

## Toleo Lililopita




## BODI YA WAHARIRI

**MWENYEKITI**
Dkt. James Andilile

**MHARIRI**
Bw. Titus M. Kaguo

**MHARIRI MSAIDIZI**
Bw. Wilfred Mwakalosi

**WAANDISHI**
Bi. Asiatu Msuya
Bi. Tobietha Makafu

**MAKAO MAKUU YA EWURA,**
Jengo la EWURA,
Kiwanja Na 3, Kitalu AD,
S.L.P. 2857, Dodoma,
Simu: +255 26 2329002-4,
Nukushi: +255 26 2329005,
Barua pepe: info@ewura.go.tz;
Tovuti https://www.ewura.go.tz
Simu ya BURE 0800110030

**Mitandao ya Kijamii**
: ewuratanzania
: ewuratanzania
: ewuratanzania
EWURA TV

# YALIYOMO

Kutoka kwa Mhariri ........................................................3
EWURA yashinda tuzo ya umahiri wa uhusiano bora na vyombo vya habari kwa mwaka 2022 .........................4
Mradi wa EACOP Tanzania wawa ndoto ya kweli............5
Rais Samia amteua Mdhibiti mbobevu Mkurugenzi Mkuu ........................................................6
Chuo Kikuu cha masuala ya udhibiti barani Afrika kuanzishwa....................................................................7
Wadau wa LPG: Mageuzi ya kisera yatachochea matumizi ...................................................................8
Tathmini ya utendaji wa mamlaka za maji waongeza ufanisi ......................................................................9
Bodi yakagua miundombinu ya kuhifadhia mafuta Dar ...10
Elimu ya leseni za ufundi wa umeme yawafaidisha wanafunzi .................................................................. 11
Maswali yanayoulizwa sana na wadau .........................12
Bodi yaidhinisha leseni 200 kwa mafundi umeme .........14



**PICHA YA MBELE:**
*Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA, Prof. Mark Mwandosya (kushoto) akipokea tuzo ya ushindi wa jumla kwa EWURA kuwa Taasisi yenye uhusiano bora na vyombo vya habari kwa mwaka 2022, tuzo iliyotolewa na Chama Cha Uhusiano Tanzania (PRST) Februari18, 2023*

# KUTOKA KWA MHARIRI



Titus M. Kaguo

**Mpenzi Msomaji wetu!**

Ninawakaribisha wote kujiunga nasi katika toleo jipya la Jarida la Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), toleo la 35 katika mfululizo wa machapisho ya majarida ya EWURA kwa mwaka 2023.

Kwa heshima na taadhima napenda kukualika kusoma makala za kuvutia kutoka katika shughuli mbalimbali za udhibiti zilizotekelezwa na EWURA. EWURA inadhibiti sekta ndogo tatu za nishati ambazo ni Petroli, Umeme na Gesi Asilia na Sekta moja ya Maji; Maji na Usafi wa Mazingira. Habari zilizoandikwa katika Toleo hili zinahusisha shughuli zilizofanyika katika kipindi cha Novemba 2022 na Febrauri 2023 na linatoka wakati EWURA ikiwa imebarikiwa na Mkurugenzi Mkuu mpya, Dkt. James Andilile baada ya uteuzi wa Rais uliofanywa tarehe 3 Februari 2023.

Katika kipindi hiki, EWURA imefanya maamuzi mbalimbali ya kiudhibiti ambayo baadhi yake, yamechapishwa katika toleo hili, ambalo linachapishwa kwa mujibu wa Sheria ya EWURA, Sura na 414 ya Sheria za Tanzania, kipengele cha 6(e)

Kipengele cha 6(e) kinasema kwamba ni wajibu wa Mamlaka kuhakikisha inaboresha ustawi wa jamii ya Watanzania kwa kuimarisha elimu kwa umma, ufahamu na uelewa wa sekta zinazodhibitiwa ikiwa pamoja na; haki na wajibu wa walaji na watoa huduma wa sekta zinazodhibitiwa; njia za kutatua migogoro na kusikiliza malalamiko, kazi na shughuli za mamlaka kwa ujumla.

Katika toleo hili pamoja na mambo mengine, habari zilizochapishwa ni pamoja na kukabidhiwa kwa kibali cha ujenzi kwa EACOP, maagizo ya EWURA kwa vituo vya mafuta matumizi ya NPGIS, Chuo Kikuu cha masuala ya udhibiti barani Afrika kuanzishwa na habari kemkem.

***Karibuni***

# EWURA yashinda tuzo ya umahiri wa uhusiano bora na vyombo vya habari kwa mwaka 2022

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imeibuka mshindi wa jumla katika tuzo za umahiri wa taasisi bora katika uhusiano na vyombo vya habari kwa mwaka 2020 katika mchujo ulioendeshwa hivi karibuni na Chama cha Maofisa Uhusiano Tanzania (PRST).

EWURA iliongoza ikizishinda taasisi kubwa mbili katika kinyang'anyiro hicho; Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Benki ya CRDB iliyoshika namba tatu.

Ilikuwa pia ni siku kubwa kwa EWURA, baada ya Meneja wake wa Mawasiliano na Uhusiano, Bw. Titus Kaguo kuibuka mshindi katika tuzo ya mwanauhusiano bora kwa mwaka 2022 katika sekta ya mafuta na gesi.

EWURA iliibuka mbele ya washindani wengine, hii ikithibitisha umuhimu wa matumizi ya utendaji bora katika uhusiano kwa masilahi ya jamii ya Watanzania katika kuongeza elimu juu ya kazi za udhibitihi.

Ni vyema ikafahamika kuwa Bw. Kaguo alinyakuwa tuzo hiyo katika kuheshimu na kutambua mchango wa kazi za uhusiano katika mashirika. EWURA inajivunia kupokea mafanikio haya ambayo hayajawahi kutokea katika masuala ya kulinda sura ya taasisi.







*KULIA: Tuzo ambayo EWURA ilishinda katika kigezo cha uhusiano bora na vyombo vya habari wakati kushoto ni tuzo aliyeshinda Bw. Titus Kaguo kama Ofisa bora wa uhusiano kwa mwaka 2022 katika sekta ya mafuta na gesi*

Akizungumzia kuhusu tuzo hizo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA, Profesaa Mark Mwandosya alisema tuzo hiyo inaipa sura mpya Mamlaka hasa ikizingatiwa ni mara chache sana mdhibiti kutambuliwa kwa kazi nzuri anayoifanya.

"Kazi nzuri Titus. Umehiheshimisha Mamlaka, endelea kusonga mbele," alisema Prof. Mwandosya kwa njia ya simu baada ya kusikia habari njema hizo katika vyombo vya habari. Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dkt. James Andilile alisema huo ulikuwa ni mwanga wa mafanikio katika shughuli za udhibiti akiongeza: "huo ni mwelekeo mzuri kwa mamlaka na hivyo basi kinachohitajika ni kubakia katika viwango vya ubora vya hali ya juu".

# Mradi wa EACOP Tanzania wawa ndoto ya kweli

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imeipa kibali cha ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) Ltd, kwa upande wa Tanzania kujenga bomba la kusafirisha mafuta ghafi katika kipande cha Chongoleani, Tanga hadi Mtukula, Kagera.

Tarehe 21 Februari 2023, EWURA ilitoa kibali cha ujenzi wa kilomita 1,115 kati ya kilometa 1,445 ya mradi mzima ambako EWURA imepewa mamlaka kisheria kudhibiti kutokana na ukweli kwamba bomba hilo linahitaji vibali kutoka sehemu mbili, EWURA kwa upande wa Tanzania na Wizara ya Nishati kwa upande wa Uganda ambayo ilishatoa kibali hicho Januari 2023.

Utoaji wa kibali hicho umekamilisha mchakato mzima wa maombi ya kibali cha ujenzi wa bomba hilo yaliyowasilishwa EWURA, tarehe 30 Juni 2022.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi kibali hicho, Mkurugezi Mkuu wa EWURA, Dkt. James Andilile alisema utoaji wa kibali hicho kumetokana na EACOP kuzingatia na kutekeleza matakwa yote ya kiudhibiti ya kutoa kibali cha ujenzi.

Waziri wa Nishati, January Makamba ndiye aliyekuwa mgeni rasmi katika hafla ya kukabidhi kibali hicho iliofanyika Dar es Salaam na kuhudhuriwa na Wakuu wa Mikoa minane ya Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga ambako bomba litapita. Pia walihudhuria Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge za Madini na Nishati na Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, Makatibu wakuu, Wajumbe wa Bodi mbalimbali, Watendaji wa mashirika mbalimbali, Menejimenti ya EWURA, waofisa wa EACOP Tanzania na waalikwa wengine katika sekta ya mafuta.



*Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dkt. James Andilile (kulia) akimkabidhi Kibali cha Ujenzi Meneja Mkuu wa EACOP Tanzania, Bi. Wendy Brown*

Katika hotuba yake fupi, Waziri wa Nishati alisisitiza kwa wakandarasi wa mradi kuheshimu matakwa ya Sera ya Uwezeshaji wa Watanzania kwa kile alichokitaja kuwa uwezeshaji wa Watanzania unaweza kuwa wa kigeni na hivyo kuwafanya Watanzania kutofaidika na Sera hiyo kama Sheria inavyotaka.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA, Profesa Mark Mwandosya alimhakikishia Waziri na Serikali kwa ujumla kuwa Bodi ya EWURA imejipanga kusimamia kiudhibiti mradi wa EACOP kuanzia kwenye hatua za ujenzi hadi utakapoanza kusafirisha mafuta kwa faida ya Wananchi wa Afrika Mashariki.

Maombi ya kibali cha ujenzi umefanywa kwa kutekeleza kipengele cha 126 cha Sheria ya Mafuta, Sura Namba 392 ya Sheria za Tanzania, pamoja na Kanuni Namba 4 (Operesheni ya bomba) ya Tangazo la Serikali Namba 477 ya mwaka 2015.

Akizungumza katika hafla hiyo, Meneja Mkuu wa EACOP Tanzania, Bi. Wendy Brown alisema: "Hii inafungua hatua nyingine mbele kwa EACOP kwa kuwa inaruhusu kuanza shughuli za ujenzi wa bomba hapa Tanzania baada ya kukamilika kwa shughuli za ukamilishaji wa masuala ya ardhi. Tunaishukuru Serikali ya Tanzania kwa kutekeleza matakwa ya utoaji wa kibali cha ujenzi kama ilivyo kwenye makubaliano ya Serikali za Tanzania na Uganda na kuendelea kutoa msaada wa utekelezajia wa mradi wa EACOP"

# Rais Samia amteua Mdhibiti mbobevu Mkurugenzi Mkuu

**Na Mwandishi Wetu**

MBOBEVU wa masuala ya Udhibiti, Dkt. James Andilile amechukua usukani kuiongoza Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kama Mkurugenzi Mkuu, baada ya uteuzi wa Rais uliotangazwa Februari 3, 2023.

Dkt. Andilile anachukua uongozi kutoka kwa Mhandisi Modestus Lumato, ambaye ni mtaalamu wa masuala ya Mafuta na Gesi aliyeteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan kuiongoza EWURA mwezi Mei, 2022.

Dkt. Andilile, mwenye Shahada ya Uzamivu wa masuala ya fedha ana uzoefu wa muda mrefu katika udhibiti baada ya kufanya kazi EWURA kama Meneja Uchambuzi wa Fedha kati ya mwaka 2008 na 2012, ambapo pamoja na kazi zingine, alikuwa anasimamia utendaji wa kifedha katika mamlaka zinazodhibitiwa, ikiwamo upangaji wa bei katika huduma.

Kabla ya uteuzi kuwa Mkurugenzi Mkuu, Dkt. Andilile alikuwa Mhasibu Mkuu katika Tume ya Pamoja ya Fedha, Wizara ya Fedha na Mipango ambapo kabla ya hapo, kati ya Aprili 2012 na Disemba 2018 alikuwa Kamishina Msaidizi wa Nishati, Wizara ya Nishati.

Kati ya Juni 2016 na Januari 2017, Dkt. Andilile aliteuliwa kuwa Kaimu Kamishina wa Nishati na masuala ya Petroli katika Wizara ya Nishati, akiwa amepandishwa cheo kutoka Kaimu Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu (PURA),



*Mkurugenzi Mkuu wa EWURA Dkt. James Andilile*

nafasi aliyoishikilia kati ya Februari 2016 na Januari 2017.

Dkt. Andilile pia alikaimu nafasi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kati ya Julai 2014 na Januari 2015. Pia alihuduma kama Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Iliyokuwa Mratibu wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PIC) ambayo kwa sasa ni Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) kati ya Novemba 2012 and Septemba 2015.

Kuja kwa Dkt. Andilile kama Mkurugenzi Mkuu wa EWUR, kutaongezea chachu utekelezaji wa shughuli za kiudhibiti kwa kuwa anaungana na wabobevu wa masuala ya udhibiti kama Prof. Mark Mwandosya, ambaye kwa sasa ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugezi wa EWURA na mwanzilishi wa mifumo ya kiudhibiti na taasisi za kiudhibiti hapa nchini.

Dkt. Andilile pia atafanya kazi na wajumbe wengine wa Bodi ya Wakurugenzi kama Bw. Haruna Masebu, mzoefu katika masuala ya udhibiti na mwanzilishi wa EWURA ambaye alihudumui kama Mkurugenzi Mkuu wa kwanza kati ya mwaka 2006 na 2013.

Mkurugenzi Mkuu mpya anatarajiwa kutumia uzoefu wa wajumbe wengine wa Bodi wazoefu katika masuala ya udhibiti kama Bw. Fadhili Manongi, Mdhibiti mwingine aliyestafu kama Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka wa Viwanja vya Ndege Tanzania

Piia Dkt. Andilile atapata msaada kutoka kwa Mhandisi Ngosi Mwihava, Naibu Katibu Mkuu Mstaafu wa Wizara ya Nishati na Bi. Victoria Elangwa ambaye ni mbobevu wa siku nyingi katika masuala ya Rasilimali Watu akiwa amehudumu katika taasisi mbalimbali za Serikali hapa nchini.

# Chuo Kikuu cha masuala ya udhibiti barani Afrika kuanzishwa

**Na Mwandishi Wetu**

CHUO cha kwanza barani Afrika chenye hadhi ya Chuo Kikuu kitakachojulikana kama *Energy Regulation Centre of Excellence* (ERCE) na kutoa elimu juu ya masuala ya udhibiti wa nishati kiko mbioni kujengwa katika Makao Makuu ya Afrika Mashariki, Arusha, baada ya Serikali ya Tanzania kupitia kwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela kukubali kutoa ardhi ya eka 10 kwa ajili ya ujenzi wa Chuo hicho cha aina yake. Hayo yalibainishwa hivi karibuni baada ya Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Profesa Mark Mwandosya kumtembelea Mkuu wa Mkoa wa Arusha, pamoja na mambo mengine kupata uhakika kutoka kwa Mkuu wa Mkoa huyo juu ya upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa taasisi hiyo kubwa ya utoaji wa elimu ya udhibiti.

Kwa sasa masuala ya elimu ya udhibiti wa nishati yanatolewa na taasisi zilizoko Ulaya na Marekani na kufanya Afrika kutumia bajeti kubwa kwa ajili ya mafunzo ya udhibiti ng'ambo.

ERCE ni kitengo kilichopo chini ya Jumuiya ya Wadhibiti wa Nishati kwa Nchi za Afrika Mashariki ambapo Makao Makuu yake yapo Arusha huku nchi wanachama wakiwa ni Kenya, Uganda, Rwanda, Sudan Kusini, Burundi, DRC na Tanzania.

Wakati wa Mkutano na Mkuu wa Mkoa, Prof. Mwandosya alisema Tanzania imepewa heshima kwa ERCE kuwa nchini, hivyo basi, kutafuta ardhi kwa ajili ya tasisi hiyo ni suala la muhimu.

"Kabla ya kuanza kujenga kituo cha mafunzo, Sekretarieti ya EREA imeagizwa kuanza kutoa mafunzo ya muda mfupi kwenye masuala ya udhibiti katika ofisi zake za sasa na baada ya Serikali kutupa ardhi, hilo litakuwa jambo la muhimu katika Mkutano wa Mwaka wa wanachama wa EREA utakaofanyika Julai Mwaka huu; na kwa bahati nzuri utafanyikia hapa Arusha," alisema Prof Mwandosya.

Kwa upande wake, RC Mongela alimshukuru Prof. Mwandosya kwa kumtembelea na kuongeza kuwa ofisi yake ina wajibu wa kufanikisha uharakishaji wa utengamano, pamoja na mambo mengine, kutoa ardhi kwa ajili ya kuanzisha taasisi za kikanda kwa maendeleo ya Afrika Mashariki.



*Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella (wa nne kutoka kulia) akiwa na Mwenyekiti wa Bodi ya EWURA, Prof. Mark Mwandosya (katikati) pamoja na Menejimenti ya EWURA na Sekretarieti ya EREA, baada ya kumaliza mkutano katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa huo*

"Tunatarajia kutoa ardhi maeneo ya Kisongo, jirani na uwanja wa ndege wa Arusha na Mungu akipenda, Mwenyekiti tutakupa mrejesho mwishoni mwa mwezi huu," alisema RC Mongela.

Kabla ya mkutano huo na Mkuu wa Mkoa, Prof. Mwandosya ambaye amebobea katika masuala ya udhibiti na mwanzilishi wa mifumo ya udhibiti na taasisi mbalimbali za udhibiti hapa nchini, alikutana na Katibu Mtendaji wa EREA, Dkt. Geoffrey Mabea, amabye alisema ERCE itakuwa ni taasisi ya kipekee na ya aina yake barani Afrika na itaipa heshima kubwa Serikali ya Tanzania.

Dkt. Mabea pia alisema ERCE itashirikiana na vyuo vingine katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kubadilishana taarifa ambazo zitasaidia katika masuala ya udhibiti. Kwa sasa EREA ina watumishi sita kutoka Rwanda, Uganda, Kenya na Tanzania na wako kwenye mchakato wa kuanda mitaaala, kupendekeza mafunzo, kuangalia mahitaji ya mafunzo, kuboresha ratiba ya wataalamu na kutafuta vyazo vya fedha.

# Wadau wa LPG: Mageuzi ya kisera yatachochea matumizi

**Na Mwandishi Wetu**

Wadau wa gesi ya kupikia (LPG) wanaiomba Serikali kuhuisha sera ili kuchochea matumizi ya gesi ya LPG kama nishati safi ya kupikia, ili kutunza mazingira na masuala ya kiafya. Wadau hao walieleza Bodi ya wakurugenzi ya EWURA wakati bodi hiyo ilipozuru mitambo ya kusindika gesi mapema Februari mwaka huu jijini Dar es Salaam kuwa serikali haina budi kuchukua hatua za kulinda mazingira ambapo wananchi watalazimika kuachana na matumizi ya mkaa na kuni kama nishati ya kupikia.

"Tunaihusisha serikali kwenye hili…kuandaa mazingira muafaka ambapo sera zetu zitahuishwa kwa kadiri inavyowezekana ili kuchochea matumizi ya LPG nchini, badala ya mkaa na kuni, kwa kuifanya gesi ya LPG kuwa bei nafuu zaidi," alisema Bw. Rizwan Sajan, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Gesi ya Manji's.

Bw. Rizwan alisema waagizaji wa gesi ya LPG wako kwenye hatua za mwisho kuunda chombo kitakachowaunganisha ili wawe na mtazamo na sauti moja kwenye masuala ya maslahi yao.

Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA ikiongozwa na Mwenyekiti wake, Prof. Mark Mwandosya, ilitembelea baadhi ya kampuni zinazoingiza gesi ya LPG nchini, ili kujionea masuala mbalimbali ya kisekta, ikiwa ni pamoja na uendeshaji, miundombinu na changamoto.

Bodi hiyo pia ilitembelea kampuni ya Taifa Gas, Kigamboni jijini Dar es Salaam, ambapo Mkurugenzi wa Uendeshaji, Bw. Stephano Mwantande alisema kuwepo kwa mazingira ya kuwa na taasisi nyingi za kudhibiti soko na shughuli za LPG ni moja ya changamoto sugu inayoumiza sekta hiyo ndogo.

> Soko la LPG nchini limeendelekea kukua katika muongo mmoja uliopita. Mwaka 2021, takwimu za gesi LPG iliyoagizwa kutoka nje zinaonyesha ongezeko la 28% kufikia tani 248,216, ikilinganishwa na tani 194,597 zilizoagizwa mwaka 2020.

"Tunazungumza na serikali ili kuangalia namna bora zaidi ya kuwa na udhibiti wa taasisi moja kwa mambo yote," alisema Bw. Mwantande na kuongeza kwamba uelewa mdogo kwa umma kuhusu faida za kupikia gesi imekuwa kikwazo katika kukochea matumizi ya bidhaa hiyo.

"Hata hivyo, Taifa Gas imekuwa ikijihusisha sana na vipindi vya elimu kwa umma ili kusaidia kukuza uelewa wa matumizi ya gesi ya LPG na faida zake," alisema.

Bodi ilijionea namna mitambo ya kujaza gesi inavyofanya kazi ili kuhakikisha kuwa makosa ya kibinadamu kama kutopima uzito kwa usahihi yanaondolewa kwa kutumia mizani maalum.

Soko la LPG nchini limeendelekea kukua katika muongo mmoja uliopita. Mwaka 2021, takwimu za gesi LPG iliyoagizwa kutoka nje zinaonyesha ongezeko la 28% kufikia tani 248,216, ikilinganishwa na tani 194,597 zilizoagizwa mwaka 2020.

Ongezeko hilo limechangiwa na ongezeko la matumizi ya gesi hiyo, kufuatia jitihada za Serikali na wadau kuhamasisha umma kupitia elimu kwa umma kuhusu umuhimu na urahisi wa kutumia LPG badala ya nishati zilizozoeleka za mkaa, kuni na mafuta ya taa.

# Tathmini ya utendaji wa mamlaka za maji waongeza ufanisi

**Na Asiatu Msuya**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) hufanya tathmini ya utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira (WSSAs) kila mwaka ili kuhakikisha kuwa, Mamlaka hizo zinatoa huduma toshelevu, zinazozingatia ubora na zenye viwango vilivyothibitishwa.Tathmini ya utendaji wa WSSAs huzingatia uwasilishaji wa mipango kazi, taarifa za utendaji za kila mwezi na mwaka, ufanisi katika usimamizi wa upotevu wa maji, usimamizi wa dira za maji, huduma kwa wateja na ufanisi katika malipo ya tozo za udhibiti.



Mkurugenzi wa Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira wa EWURA, Mha. Exaudi Fatael, ameeleza kuwa, lengo la tathmini hiyo ni kuhakikisha mamlaka zinatekeleza majukumu yao ipasavyo kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo iliyopo, kujali maslahi ya wateja na kutumia rasilimali zake kuimarisha ubora na ufanisi wake wa utoaji huduma.

"Tathmini hizi zimechochea kuimarika ufanisi na ubora wa huduma zinazotolewa na mamlaka za maji, hali ya upatikanaji huduma na kuendelea kuimarika kwa uzalishaji maji sanjari na kupungua upotevu wa maji,"alisisitiza Mha. Fatael.

Kwa 2023, EWURA itazindua ripoti ya 14 ya utendaji wa tathmini wa mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira za mikoa, miradi ya kitaifa na mamlaka za wilaya na miji midogo. EWURA hutekeleza jukumu hili kwa kwa mujibu sheria ya EWURA, Sura Na 414; na sheria nyingine zinazoisimamia sekta ya maji nchini.

Hivyo basi, Mamlaka za maji zinatakiwa kuendelea kuwasilisha kwa wakati ripoti za utendaji wao wa kila mwezi na mwaka, kuandaa na kutekeleza mikakati ya kupunguza upotevu wa maji, kuwafungia wateja dira za maji zilizokaguliwa na kuthibitishwa na mamlaka husika na kuongeza wigo wa utoaji huduma kwa wateja wao.

Aidha, Mamlaka zinapaswa kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kulipa tozo za udhibiti kwa ufanisi, kutunza rekodi ya malalamiko ya wateja sanjari na kufanya tathmini ya namna wateja wao wanavyoridhishwa na huduma zinazotolewa.

Vilevile, Mamlaka zinapaswa kutenga eneo maalumu la kuchakata, kutibu na kuhifadhi majitaka, mwongozo wa usimamizi majitaka na sera ya usimamizi wa dira za maji.

EWURA inao wajibu kisheria kudhibiti kiufundi na kiuchumi utoaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira nchini kupitia Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira kwa kutoa leseni za uendeshaji, kusimamia ubora wa huduma na kutathmini na kupitisha maombi ya bei za huduma.

# Bodi yakagua miundombinu ya kuhifadhia mafuta Dar

**Na. Tobietha Makafu**

Bodi ya wakurugenzi ya EWURA imefanya ziara ya kikazi katika miundombinu ya kuhifadhia mafuta ya TIPER, iliyopo eneo la Kigamboni, Dar es Salaam, ili kujionea kazi, maendeleo na changamoto mbalimbali inayoikabili kampuni hiyo. Akizungumzia ziara hiyo, Mwenyekiti wa Bodi ya EWURA, Prof. Mark Mwandosya, alisema, EWURA imefanya ziara hiyo ili kufahamu kiundani, utekelezaji wa majukumu mbalimbali, mafanikio na changamoto ya uhifadhi wa mafuta ili EWURA iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na tija kwa Taifa kwa ujumla.



*Waziri wa Nishati, January Makamba (kushoto) akipokea nakala ya kibali cha ujenzi kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya EWURA, Prof. Mark Mwandosya wakati wa hafla ya kukabidhi kibali hicho kwa EACOP Tanzania iliyofanyika Dar es Salaam tarehe 21 Februari 2023*

Akifanya wasilisho juu ya utendaji wa kampuni hiyo, Kaimu Meneja wa TIPER, Bw. Martin Mosha alisema: "TIPER ipo kimkakati, ili kuhakikisha nchi inakua na hifadhi ya mafuta ya kutosha kwa matumizi ya nchini na baadhi ya nchi zinazotegemea kupitisha mafuta nchini, kama vile Zambia, Kongo, Malawi na Burundi.

"Kwa sasa TIPER ina ukubwa wa eneo wenye Hekta 58 na maghala 32 yenye uwezo wa kuhifadhi lita milioni 253 za mafuta, zikiwa zimeongezeka kutoka lita milioni 140 ilivyokuwa wakati inaanza kazi mwaka 1999"

Ujumbe kutoka EWURA uliongozwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Prof. Mark Mwandosya na wajumbe wa Bodi hiyo ambao ni pamoja na aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mha. Modestus Lumato, Mr. Fadhil Manongi, Mha. Ngosi Mwihava, Bi. Victoria Elangwa, Dr. James Andilile and Mr. Haruna Masebu.

EWURA ina jukumu la kusimamia mkondo wa chini na kati wa Sekta ndogo ya Mafuta Tanzania Bara, kiufundi na uchumi pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa za petroli nchini wakati wote ili kuboresha gharama katika ununuzi, uhifadhi, usafirishaji na usambazaji wa bidhaa za petroli.

Kampuni ya TIPER ilitokana na kiwanda cha AGIP cha kusafisha mafuta kilichojengwa mwaka 1966 ambacho kilifungwa mwaka 2000 na maghala yake kuwa ni moja ya eneo kubwa ya kuhifadhia bidhaa za petroli.

Kwa mujibu wa ripoti ya utendaji wa sekta ya petroli ya mwaka 2021, Tanzania ina jumla ya maghala 29 ya kuhifadhia mafuta yenye mita za ujazo 75,625, zinazomilikiwa na kampuni mbalimbali kama vile, Afroil investment, Camel Oil Ltd, G & M Co Mtwara, Gapco (T) Ltd, GBP (T) Ltd, Hass Petroleum Ltd, Lake (T) Ltd, Lake Oil Ltd, MOIL, Oilcom (T) Ltd, Oryx Oil Ltd.

Nyingine ni Puma Energy (T) Ltd, Sahara (T) Ltd, Star Oil (T) Ltd, Superstar Forwarders Co Ltd, Vivo Energy na World Oil.

# Elimu ya leseni za ufundi wa umeme yawafaidisha wanafunzi

**Na Tobietha Makafu**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imetoa elimu ya leseni kwa mafundi umeme kwa wanafunzi wa Chuo cha Ufundi cha Arusha (ATC) na Chuo cha Ufundi Stadi cha Veta Arusha, na kuwataka wanafunzi hao, kuwa na leseni ya ufungaji wa mifumo ya umeme inayotolewa na EWURA ili wafanye kazi hizo kwa mujibu wa sheria.

Akitoa mafunzo hayo Meneja wa EWURA Kanda ya Kaskazini, Mha. Lorivii Long'idu alisema, semina hiyo imelenga kutoa elimu kwa wanafunzi wanaosomea fani ya umeme ili kuwakumbusha wajibu wao watakapohitimu mafunzo yao na kuifahamu vyema EWURA.

Alisema, Serikali imewekeza nguvu kuhakikisha huduma ya umeme inafika katika vijiji vyote nchini, hivyo kutakuwapo na uhitaji wa mafundi umeme kwenda kufanya kazi sehemu hizo, elimu hii itawafanya wafahamu matakwa ya kisheria, ikiwemo namna ya kuomba leseni za ufungaji wa mifumo ya umeme.

"Natoa onyo kwa vishoka wote, kuacha mara moja kujishughulisha na kazi ambazo hawajazisomea, rai yangu waende kwenye vyuo vya ufundi, wajisajili kwa lengo la kujifunza ufundi wa umeme kwa kuwa nchi inaongozwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na utaratibu" alisema Mha. Lorivii.

Akizungumza wakati akifungua mafunzo hayo, Mkuu wa Chuo cha ufundi Arusha,



Dkt. Mussa Chacha alisema, chuo hicho ni miongoni mwa vyuo vinavyozalisha vijana waliobobea katika sekta ya umeme ambapo aliishukuru EWURA kwa elimu hiyo itakayowasaidia vijana hao.

EWURA imetoa elimu kwa wanafunzi hawa, kwasababu wao ni nguvu kazi inayotarajia kuingia kwenye ajira, hivyo wanapaswa kufahamu kanuni, taratibu na sheria zinazopaswa kufuatwa wakiingia kazini.

Mha. Lorivii aliendelea na kusema "Kwa mujibu wa sheria ya umeme ya mwaka 2008 na Kanuni za ufungaji wa mifumo ya umeme ya mwaka 2019, ni kosa kisheria kufanya shughuli za ufungaji wa mifumo ya umeme bila kuwa na leseni ya EWURA.

Akizungumzia sababu kwanini wamefanya semina hiyo, Mha. Lorivii alisema, katika kaguzi mbalimbali zilizofanywa na EWURA, imegundulika uwepo wa mafundi wengi wa umeme, kufanya kazi bila ya kuwa na leseni na wengine wanayo elimu ya ufundi lakini hawajui taratibu za kupata leseni hizo.

"Serikali ya awamu ya sita, ipo katika mpango wa kupeleka umeme vijiji vyote nchini, kwahiyo tutakuwa na uhitaji mkubwa wa mafundi umeme kwenda kusaidia katika ufungaji wa mifumo ya umeme, katika majumba ya watu na sehemu tofauti, ni vyema wanafunzi hawa wakajua umuhimu wa leseni kwa ajili ya shughuli hizi.

EWURA ina jukumu la kusimamia shughuli za Sekta ndogo ya Umeme, ambazo zinatakiwa kufanywa na mafundi umeme wenye leseni, Hivyo ni utaratibu wa kawaida kuwaelimisha wadau ili kuimarisha usalama wa raia na mali zao.

# Maswali yanayoulizwa sana na wadau

**Na Mwandishi wetu**

Ndugu msomaji, katika toleo hili tunakuletea baadhi ya maswali ambayo huulizwa sana na wadau mbali mbali ili kupata uelewa wa mambo mbali mbali yanayohusu EWURA. Ni matarajio yetu kuwa, majibu ya maswali hayo yatakusaidia msomaji au mtu mwingine yeyote atakayetaka kufahamu kutoka kwako.

### 1. EWURA ni nini?

EWURA Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji. Kwa upande wa Nishati, EWURA inadhibiti huduma za Mafuta ya jamii ya petroli, Gesi Asilia na Umeme, na upande wa Maji inadhibiti mamlaka za Maji za Mikoa, Wilaya, Miji mikuu na Miradi ya Kitaifa. Udhibiti unafanywa ili kuhakikisha kwamba huduma zote zinazodhibitiwa, zinakidhi viwango vya kitaifa na kimataifa, na zinatolewa kwa gharama inayostahili. Hii ni muhimu ili kumlinda mtumia huduma na mtoa huduma. Wasipolindwa hawa, yeyote anaweza kumtendea mwingine isivyostahili.

### 2. Mtoa huduma na wanaopokea huduma wanalindwaje?

Mtoa huduma analindwa kwa kusimamia sheria, sera, kanuni na taratibu zinazompa uhakika wa kulindwa na kuifanya biashara yake kuwa endelevu. Vile vile, mdhibiti anapaswa kuidhinisha bei zinazoakisi gharama halisi za huduma, ikiwa ni pamoja na faida kwa mtoa huduma ili kulinda mtaji wake. Mtoa huduma pia analindwa dhidi ya uonevu unaoweza kufanywa na watoa huduma wenzake au maamuzi ya kisiasa yasiyo haki.

Mtumia huduma analindwa kwa kuhakikisha kuwa kunakuwa na mkataba wa huduma kwa wateja, ili kuweka bayana wajibu na haki baina ya pande mbili hizo. Mpokea huduma pia anapewa fursa ya kuwasilisha malalamiko dhidi ya mtoa huduma, kwa lengo la kusuluhisha na kufanya maamuzi ya haki, ikiwamo fidia pale inapostahili. Ni kwa manufaa ya mpokea huduma pia kuhakikishiwa uwepo wa huduma kwa namna bora na kwa bei stahiki.

### 3. Kuna utitiri wa vituo vya mafuta vimejengwa kwenye makazi ya watu. Nini mtazamo wa EWURA kuhusu hili?

Kisheria, ujenzi wa vituo unatakiwa kufuata mambo haya; kuzingatia mipango ya miji; kuepuka athari za kimazingira, kufuata taratibu za ujenzi wa majengo, kufuata taratibu za huduma za zimamoto na uokoaji, na kufuata matakwa ya kiafya, kiusalama, na kimazingira. Matakwa haya yote husimamiwa na serikali kupitia taasisi zake mbalimbali. EWURA inaratibu hatua ya mwisho ya kuhakikisha maombi ya kibali cha ujenzi yamezingatia idhini kutoka taasisi husika kwenye maeneo yaliyotajwa.

Hata hivyo, ni vema ikaeleweka pia kwamba vituo vya mafuta vinajengwa kukidhi mahitaji ya watumiaji yanayoongezeka kwa kasi. Katika hali halisi kwa sasa, mathalan, je, watumia huduma wangependa kwenda umbali wa kilomita tatu au tano kufuata mafuta, au Kwenda nje ya mji kufuata mafuta?

Pamoja na vituo vya mafuta kuwa vingi, EWURA inasimamia kwa karibu ujenzi bora wa miundombinu yake ili kudhibiti hatari inayoweza kuleta madhara inapotokea ajali ya moto. Vituo vya mafuta, licha ya kuwa vinajengwa mitaani, matenki yake huwekwa ardhini, hivyo kupunguza sana uwezekano wa ajali ya moto kwa matenki hayo; tofauti na maghala ya kuhifadhia mafuta ambayo huwekwa juu ya ardhi na kuwa hatarishi zaidi. Ni kwa sababu hii basi, maghala ya namna hii huwekwa sehemu maalum ambazo ni mbali kabisa na makazi ya watu.

### 4. Udhibiti wa biashara ya mafuta unakuwaje?

Udhibiti wa nishati ya mafuta hufanywa kwa kutoa leseni kwa yeyote anayekidhi vigezo vya kufanya biashara hii. Leseni inatoa masharti ya kufuata wakati wote. Na hayo ndiyo tunayosimamia. Masharti hayo ni kama kuuza bidhaa zenye viwango, kuuza kwa kufuata bei elekezi, kuhakikisha miundombonu inakuwa imara wakati wote nk.

### 5. Ni kwa nini vituo vya mafuta vina bei zisizofanana, hali ambayo huleta usumbufu kwa watumiaji kwa kila kituo kuwa na bei yake?

Bei za mafuta hutokana na gharama ambazo muuzaji anakuwa ametumia kuyapata, pamoja na faida anayotakiwa kuipata kisheria. Sasa wawekezaji wanaweza kuwa na gharama zinazotofautiana katika uendeshaji wa biashara yenyewe. Wengine wanabana matumizi, wengine wanaendesha kawaida. Wengine wana wafanyakazi wengi, na walipa mishahara mikubwa, wengine wanao wachache na mishahara ya kawaida.

Wengine pia hukodisha magari ya kubeba mafuta hayo, lakini wengine wana magari yao kwa ajili ya kazi hiyo. Kutokana na tofauti katika gharama kama hizo, wakati mwingine mfanyabiashara anapata fursa ya kutoa punguzo baada ya kujihakikishia gharama za uendeshaji kwake ni ndogo, na punguzo hilo pia linamsaidia kupata wateja zaidi kuliko mshindani wake. Kwa EWURA, huu ni ushindani wa haki, ambao pia unampa fursa mtumiaji kuchagua wapi akapate bidhaa kwa bei anayoimudu. Ndiyo msingi mkuu wa soko huria kujenga ushindani wa haki.

### 6. Ni kwa nini siku hizi kila bei za mafuta zikipanda sababu inayotolewa na Vita ya Ukraine na Urusi ilhali mafuta yetu hayatoki huko?

Kuna gharama nyingi zinazochangia kwenye bei za mafuta. Baadhi ni gharama za kunulia na kusafirishia mafuta, bima ya shehena ya mafuta, gharama za kununulia fedha za kigeni zinazotumika kununulia mafuta, kodi za serikali, tozo za taasisi zinazohusika kusaidia upakuaji wa shehena za mafuta, faida ya waagizaji na gharama za usafirishaji kutoka kwenye maghala.

Urusi ni moja ya watoaji mafuta kwa wingi ulimwenguni. Kutokana na sababu za kisiasa, nchi nyingi zimesusa kununua mafuta yake. Hili limesababisha nchi hizo kwenda kwenye masoko mengine ambako uzalishaji umekuwa wa kiwango kile kile licha ya mahitaji kuongezeka.

Hali hii ndiyo imesababisha bei kupanda kwenye masoko hayo. Ikumbukwe pia kwamba, mahitaji mengine katika eneo hilo kama meli za usafirishaji mafuta na huduma za bima yamekuwa ghali sana kwa sababu hizo hizo.



# Bodi yaidhinisha leseni 200 kwa mafundi umeme

**Na Asiatu Msuya**

Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imeidhinisha kwa mkupuo moja leseni 203 za huduma ya ufungaji umeme kwa mwezi Januari 2023. Leseni hizo ni pamoja na sita za daraja A, leseni 8 za daraja B na leseni 134 za daraja C. Bodi hiyo pia imeidhinisha leseni 55 za Daraja D. Kati ya leseni 203 zilizotolewa, 192 ni za wanaume na 11 ni wanawake.

Mapendekezo ya utoaji wa leseni huzingatia miongozo ya kutoa leseni kwa wataalamu wa ufungaji mifumo ya umeme, sifa za kitaaluma na uzoefu wa waombaji kama zilivyoainishwa na Kanuni za Umeme (Huduma za Ufungaji Umeme) za Mwaka 2022.



Akizungumzia suala hilo, Kaimu Mkurugenzi wa Umeme wa EWURA, Mha. Erick Rugabera alisema, EWURA hutoa leseni kwa mujibu wa kifungu cha 8(1) (h) cha Sheria ya Umeme, Sura ya 131, inayowataka mafundi umeme wote kuomba na kupata leseni kutoka EWURA kabla ya kufanya shughuli za ufungaji wa umeme.

"Leseni zinazotolewa na Mamlaka zitatumika Tanzania Bara na zinampa mwenye leseni uwezo wa kufanya shughuli za ufungaji umeme nchini kote, huhuishwa kila baada ya miaka mitano," alisisitiza Eng. Rugabera.

Leseni ya Daraja A hutolewa kufanya kazi za ufungaji wa umeme katika misongo ya volti zote; Daraja B katika msongo wa hadi Volti 33,000 wakati Daraja C hutolewa kufanya kazi za ufungaji wa umeme wa msongo wa hadi Volti 1000.

Aidha, Daraja D hutolewa kufanya kazi za ufungaji wa umeme wa msongo wa hadi Volti 230; Daraja W kufanya kazi za umeme chini ya wasimamizi walio na leseni za Daraja A, B, C,S1,S2,S3 au D huku Daraja la S1 likiwa maalum kwa ufungaji umeme katika misongo yote.

Vilevile, Daraja S2 hutolewa kufanya ufungaji maalum wa umeme hadi volti 33,000; na S3 ni hadi volti 1,000.

Maombi ya leseni hufanywa mtandaoni kupitia Mfumo wa Taarifa za Leseni unaopatikana unaojulikana kama LOIS katika tovuti ya EWURA www.ewura.go.tz kupitia kiunganishi https://lois.ewura.go.tz/ewura/.

Maombi hayo huambatana na nakala za vyeti vya kitaaluma vya mwombaji; wasifu wake, picha ya rangi ya pasipoti iliyochukuliwa hivi karibuni yneye kivuli cha rangi ya bluu; kibali cha kazi husika kwa waombaji wasio raia; ada ya maombi isiyorejeshwa na nambari halali ya utambulisho wa mlipa kodi (TIN).